


## MAELEKEZO YA KUTENGENEZA KADI YA MPIGA KURA

1. Jaza taarifa za Mpiga Kura katika kadi ya Mpiga Kura
2. Mpiga Kura aweke saini yake na Mwandishi Msaidizi aweke saini yake.
3. Bandika picha ya Mpiga Kura katika sehemu ya kuweka picha iliyoko kwenye kadi katika fomu kwa kutumia gundi kidogo.
4. Kata kadi ya Mpiga Kura.
5. Shika kifuko maalum cha plastiki cha kutengenezea kadi upande wenye plastiki ukiwa mbele yako.
6. Pinda kidogo katika kona moja ya kifuko hicho ili karatasi ibanduke.
7. Bandua karatasi katika upande mmoja wa kifuko hicho.
8. Weka kwa uangalifu kadi katika sehemu uliyobandua karatasi na uhakikishe kadi imekaa ndani vizuri.
9. Ondoa karatasi upande wa pili uliobaki wa kifuko maalum cha plastiki.
10. Kunja kifuko hicho katikati kwa kufuata mstari ulioko katika kifuko hicho.
11. Tumia kimwiko kidogo cha plastiki ulichopewa kusugulia kadi ili ikae vizuri kwa kunyooka.

## MAELEKEZO

Kubandika Picha

Kwanza ondoa karatasi iliyogandishwa kwenye FotoFix Film ili kupata sehemu ya gundi.

Weka picha yako kwenye chumba cha ndani kilichoandikwa "PICHA" halafu gandisha FotoFix Film ukihakikisha haivuki mistari iliyo katika doti doti.